# UHAKIKI WA DINI NO.5

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

UHAKIKI WA DINI NO.5

.UHAKIKI WA DINI KUPITIA MSINGI WA IJTIHADI

Katika makala iliyopita, tulielezea umuhimu wa uhakiki wa dini kupitia msingi wa Ijtihadi, katika makala hiyo tulielezea misingi mitatu inayoweza kumuongoza mwanaadamu katika uhakiki .wake wa dini, katika makala hii tutaendelea kuelezea misingi mengine ya uhakiki wa dini

Kutambua falsafa ya dini, ikiwa kama ni moja ya misingi ya dini kunaleta athari nyingi nzuri .9 katika taaluma za dini, na dalili bora inayothibitisha kutokuwepo sawa wanaadamu duniani na -:(Akhera ni kutokana na daraja ya elimu waliyonayo, kama anavyosema Allah (s.w

[1]"اَمَّنْ هُوَ قَانِتٌ آنَاء اللَّيْلِ سَاجِداً وَقَائِماً يَحْذَرُ الآخِرَةَ وَيَرْجُو رَحْمَةَ رَبِّهِ قُلْ هَلْ يَسْتَوِى الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِين لاَ يَعْلَمُونَ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُوْلُوا الاَلْبَابِ"

Je, afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo)? Sema: “Je, wanaweza kuwa .sawa wale wanaojua na wale wasiojua?” wanaotanabahi ni wale wenye akili tu

Taaluma ya dini ndio inayomfanya mwanaadamu awe mtiifu katika maisha yake ya duniani na ,kumfanyia wepesi baada ya kufa

" معرفة العلم دين يدان به به يكتسب الانسان الطاعة في حياته و جميل الآحدوثة بعد وفاته "

Kupitia elimu na maarifa ya dini mwanaadamu anakuwa na dini, na kupitia elimu hiyo mwanaadamu anakuwa mtiifu katika maisha yake, na matokeo mema ni baada ya kufariki .kwake

(Na katika hadithi nyengine anasema: Maulamaa wa dini ndio warithi wa Mitume (a.s

" العلماء ورثة الأنبياء "

.Yaani: Maulamaa ndio warithi wa Mitume

Basi ni lazima kuitambua falsafa ya dini ili tunufaike na athari nyingi zisizo mpaka ambazo .hupatikana kutokana na taaluma za dini

Hiyo ilikuwa ni misingi ya uhakiki wa dini, tunategemea tutakuwa tumenufaika na maelezo .hayo

.Surat Azzumar Aya ya 9 [1]

MWISHO